**Noa Bongo – Jenga Maisha Yako - Utandawazi : Biashara ya Pamba Burkina Faso**

**O-Ton : Yahya Boudani**

**Text : Sandrine Blanchard**

**Reaktion : Yann Durand**

**Übersetzung : Anne Thomas**

---

**3 Stimmen ……..Sauti 3**

**- junger Sprecher 1……..Msimulizi wa kiume 1**

**- junge Sprecherin 1…… Msimulizi wa kike 1**

**-Sprecher(in) 2 …………Msimulizi wa kike 2**

**als Off –Stimme für die Reportage.**

**Für die O-Tone dazu 2 Männer ,1 Frau :**

- **Vorsizende d .Kooperative ………Mkuu wa Ushirika**
- **Bauerin …………………Mkulima wa kike**
- **Helvestas – Vertreter ………..Wakala w Helevestas**

---

**Vorspann LbE………………Kiashirio cha Kipindi**

**SEHEMU YA KWANZA – REPORTAGE : REPOTI**

**Msimulizi wa kike 1 :**Habari ! Hamjambo wote

**Msimulizi wa kiume 1** : Leo katika mfulilizo wa vipindi vyetu vya Utandawazi tutazungumzia juu ya kilimo cha mbolea ya asili na biashara inayozingatia haki.

**Msimulizi wa kiume 1 :** Tutakuwa tunaelekea ……. Burkina Faso taifa linalozalisha pamba kwa wingi kabisa barani Afrika.

**1: Atmosphere Auto unterlegen ………**

**Msimulizi wa kiume 1** : Kwa kufafanua zaidi hasa tutakuwa tunaelekea katika jimbo la Bazega lilioko kama kilomita 70 kusini mwa mji mkuu wa Ouadougou.

**Msimulizi wa kiume 1 + Msimulizi wa kike 1 :**
Kwa hiyo fungeni mikanda yenu tayari kwa safari!

**…………………Manuskript…………………….**

**1.Atmosphere Auto hoch…………………**
**Msimulizi wa kike 2 :** Kuondoka kutoka Ouagadougou inachukuwa masaa mawili kuweza kuwasili katika kijiji cha Goumsin. Baada ya kusafiri kwa kitambo fulani njia inazidi kuwa mbaya na inakuwa vigumu kuendesha gari kwa hiyo sehemu ya mwisho ya safari inabidi ifanyike kwa miguu.

**2. Atmo Schritte unterlegen……….**

**Msimulizi wa kike 2 :** Konde zote zilizotuzunguka zimekauka …Wakati wa mavuno umemalizika.

**3.Atmo Gespräch hoch und unterlegen ………..**

**Msimulizi wa kike 2 :** Hapa katika kijiji cha Goumsin wakulima wa pamba 127 wamaeanzisha ushirika wa uzalishaji wa pamba ujulikanao kama Laafi la Bambou.Wameamuwa kutumia kilimo cha mbolea ya asili jambo ambalo linamaanisha kwamba wamekataa kutumia mbolea za kemikali na badala yake kutumia njia za kilimo za asili zaidi.Nikiema Mathew ni rais wa ushirika huo wa Laafi la Bambou.

**4.Nikiema Mathew – Vortelle**
Faida ya kwanza ya kilimo cha kutumia mbolea ya asili ni kuhusiana na afya yetu.Wakati tulipokuwa tukiyanyunyiza mashamba madawa ya kuulia wadudu waharibifu wa mazao yumkini huishia kitandani kwa siku tatu kwa sababu ya gesi za madawa hayo.Tulikuwa tukiteseka sana.

**Msimulizi wa kike 2 :**
Katika jimbo la Goumsin asilimia 57 ya wakulima wa kilimo cha mbolea ya asili ni wanawake na Suzanne Zougrana ni mmoja wao. Ameukaribisha ukulima huo wa asili ambao sio tu unahakikisha kuzalisha mazao bora bali pia umechangia katika suala la kuwakombowa wanawake.

**5. Zougranne Suzanne ---Fauen ; ……………………..**
Wanawake huwa wanalima mashamba yao wenyewe kwa hiyo kunakuwa hakuna haja ya kuwategemea waume zao.Iwapo mume anauza pamba yake na kumfikiria mkewe hilo ni jambo zuri lakini iwapo anakataa kumpa mkewe vijisenti kidogo hilo haliwi tatizo.Kwani mke anakuwa na shamba lake mwenyewe anaweza kufaidika na matunda ya kazi yake mwenyewe.Halazimiki tena kumtegemea mume wake na anaweza kufanya maamuzi yake mwenyewe juu ya matumizi yake.

**Msimulizi wa kike 2 :** Kwa hiyo huko Goumsin wanawake wamekuwa ndio ingini ndio msukumo wa nguvu kuu ya ukulima wa asili.

**Msimulizi wa kiume 1 (akicheka ) :**
Wanawake ni ingini….ni jambo la kufurahisha!

**Msimulizi wa kike 1 (anaonekana kukereka ) :**
Hebu huwezi kunyamaza ? Suzanne alikuwa akielezea kwa nini wanawake ni muhimu sana ……kushinda wanaume !

**6.Zougranna Suzanne – Bio**
Tumeachana na utaratibu wa kawaida wa kilimo cha pamba kwa sababu kazi ilikuwa ngumu mno kwa wanawake.Sisi wanawake tulikuwa hatuwezi kutumia kemikali kwa ajili ya kuuwa wadudu kwenye pamba .(Anacheka ) Mwanamme mmoja amesema kwamba ni mke wake ndie aliyemuingiza kwenye kilimo cha kutumia mbolea ya asili ……katika matukio mengi ni wanawake ambao huanza na ukulima wa asili wakifuatiwa na waume zao.

**Msimulizi wa kike 2 :** Pamba inayolimwa kwa kutumia mbolea ya asili hugharimu zaidi kuliko pamba ya ukulima wa kawaida.Na hata kama mavuno yake yanakuwa kidogo wakulima wake wanakuwa na kipato cha uhakika.Nikiema Mathew anaelezea :

**7. Nikiema Mathew – Preise :** Iwapo utazalisha tani moja ya pamba ya ukulima wa kawaida na kilo mia nne au tano za pamba ya kilimo cha asili bado utakuta unajipatia fedha zaidi kutokana na pamba ya asili .Kwa kilimo cha mbolea ya asili unavuna kile ulichokipanda na unakuwa huna haja ya kutowa chochote kwa kampuni za kemikali.

**8.Atmo Ouagaduogou Strase- hoch dann unterlegen ……..Mtaani Ouagadougou …………………**

**Msimulizi wa kike 2 :** Tumerudi tena Ouagaduogou.Ushirika wa Laafi la Bambou una uhusiano na shirika lisilo la kiserikali la Uswisi linaloitwa Helvetas ambalo lina ofisi yake mjini Ouagadougou.Helvetas linashirikiana na Umoja wa Wakulima wa Pamba wa Taifa wa Burkina Faso UNPCB.

**9 .Helvetas**
Jina langu ni Ouedraogo Abdoullaye mimi naongoza tawi la Helvtas la kilimo cha asili nchini Burkina Faso.Tuna mpango wa kuwasaidia wakulima.Mpango huu huwapatia wakulima wadogo wadogo zana za kisasa zaidi.Helvetas pia hushirikiana na shirika la Kijerumani HessNatur ambalo hujishughulisha maalum na katika biashara inayozingatia haki na kilimo cha asili.

**10. Helvetas – HessNatur**
Tuna kondarasi za muda mrefu na washirika wetu wa Ujerumani kama vile HessNatur wakituhakikishia kununuwa pamba. Mpango huo pia unasaidia miradi ya kijamii kama vile elimu kwa wasichana.Shirika la HessNatur linasaidia elimu katika kila ngazi ya Umoja wa Wakulima wa Pamba nchini Burkina Faso UNPCB . Hivyo ndivyo pamba ya Burkina Faso inavyoingia Ujerumani ….mara tu baada ya kutengenezwa kuwa nguo.Wazungu ambao huenda hawakuwahi kuona mti wa pamba katika maisha yao huvaa nguo za pamba ya Burkina Faso.

## MWISHO WA SEHEMU YA KWANZA

**Music hoch dann unterlegen und ausblenden…………**

**SEHEMU YA PILI ERKLÄRSTÜCK ……….**
**Msimulizi wa kiume 1 na Msimulizi wa kike 1 tu ! :**

**Msimulizi wa kiume:** Fikra ya kilimo cha asili ni ya kuvutia inamaanisha wakulima wana kipato cha uhakika wakati huo huo wakizalisha mazao ya kiwango bora………Lakini katika repoti tuliyoisikia juu ya pamba na biashara inayozingatia haki kimsingi ni aina ya biashara mbadala au sivyo ?

**Msimulizi wa kike:** Ndio, ni mbadala kwa biashara katika maana halisi.Lengo ni kuwawezesha wakulima katika nchi za kimaskini kujipatia fedha zaidi kwa kuuza mazao yao.

**Msimulizi wa kiume:** Lakini biashara inayozingatia haki hasa inafanya kazi vipi ?

**Msimulizi wa kike:** Wakulima katika nchi zinazoendelea kwanza inabidi waanzishe ushirika wa kidemokrasia na ulio huru.Katika repoti tumeweza kusikia juu ya ushirika wa Laafi la Bambou.Baadae wakulima inabidi waje na lengo la pamoja ..hiyo ina maana kwamba inabidi watafute njia ili jamii nzima ifaidike na fedha wanazopata kutokana na kuuza mazao yao.

**Msimulizi wa kiume:** Sio rahisi hivyo.

**Msimulizi wa kike:** Huwa wanaweza kupata msaada kutoka mashirika yasio ya kiserikali kama vile Helvetas ambalo hivi punde tu tumepata habari zake.Mara ushirika unapoundwa huwa unafanyiwa ukaguzi.

**Msimulizi wa kiume :**…na nani ?

**Msimulizi wa kike:** Na FLO yaani Shirika la Kimataifa la Kutowa Cheti cha Biashara Inayozingatia Haki …ambalo hukakikisha kwamba kanuni zinaheshimiwa.

**Msimulizi wa kiume :**Kama vile kiwango cha ubora wa mazao,njia za mavuno na mishahara wanayopata wakulima.

**Msimulizi wa kike :** Ndio na shirika la FLO linaweza kuamuwa kuupa ushirika alama ya Biashara inayozingatia haki.

**Msimulizi wa kiume :** Kwa hiyo ili kupata cheti wakulima inabidi waepuke kutumia madawa ya kuuwa wadudu waharibifu wa mazao au mbolea za kemikali.

**Msimulizi wa kike :** Kuwa mwangalifu kidogo hapa biashara inayozingatia haki haimaanishi kwamba kilimo lazima kiwe cha asili…..biashara inayozingatia haki kwa kiasi kikubwa huendeshwa kwa kutilia maanani maslahi ya kijamii.

**Msimulizi wa kiume ;** Hiyo ina maana kwamba wakulima wadogo hupatiwa hakikisho kwa mazao yao ?

**Msimulizi wa kike :** Ndio bei huwa zinapangwa na mapema ili kwamba wakulima wanakuwa hawategemei soko la dunia.Biashara inayozigatia haki pia humuweka kando mtu wa kati ambaye anakuwa kama mlanguzi na kunakuwa na hatua chache za kufuata kuanzia uzalishaji hadi mauzo na fedha zaidi huwa zinaachwa kwa mkulima.

**Msimulizi wa kiume :**Jambo hilo linaleta maana ! Lakini hebu niambie umetaja neno mauzo …wapi hasa naweza kununuwa bidhaa za biashara inayozingati haki ? Vipi zinaweza kutambulika?

**Msimulizi wa kike :** Kwanza inabidi ukumbuke kwamba bidhaa za biashara inayozingatia haki bado huwa ni bidhaa zenye kufaa katika biasahara duniani.Nchini Ujerumani bidhaa 2,500 zina alama ya biashara inayozingatia haki.Lakini kujibu suali lako bidhaa hizo zinaweza kununuliwa katika maduka maalum ambayo mara nyingi huwa yanaitwa maduka ya dunia na nyingi zaidi ya bidhaa hizo

unaweza ukazipata kwenye maduka makubwa ya bidhaa. Kuna nembo ya kimataifa kuweza kuzitambuwa bidhaa za biashara inayozingatia haki.

**Msimulizi wa kiume :** Kile nilichokisikia ni kwamba wabunge wa Ujerumani wanaweza kula bidhaa za biashara inayozingatia haki katika mkahawa wa bunge mjini Berlin. Juu ya kwamba tukizungumzia kwa ujumla bidhaa za biashara inayozingatia haki ni za ghali zaidi kuliko bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia njia za kawaida ambapo gharama zake huwa juu kwa zaidi ya asilimia 15.

**Msimulizi wa kike :** Lakini mashabiki wa biashara yenye kuzingatia haki wao wangelisema hiyo ni gharama ili kulipia kuwa na maadili na mshikamano zaidi.

**Outro …Funga Kipindi**

Na hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi chetu hiki cha Noa Bongo - Jenga Maisha Yako………Asante kwa kusikiliza kipindi hiki juu ya utandawazi : kilimo cha asili na biashara inayozingatia haki. Ni kipindi cha Deutsche Welle kilichotayarishwa na Yaya Boudani na Sandrine Blanchard. Ili kujuwa zaidi au ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki tafadhali nenda kwenye tovuti yetu www.dw-world.de/be
Usikose kujumuika nasi tena mara nyengine !
Kwaheri!